JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAŶANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya Simu:
Simu:. 2756204
E-mail:mandakatc@gmail.com
Fax:027-2756204
Simu:- 0754867064

CHUO CHA UALIMU MANDAKA,
S.L.P.725,
MOSHI.

Unapojibu tafadhali taja:

Tarehe 23 AGOSTI, 2016

KUMB.NA.MTC/ST/21/VOL.V/74

JINA:-.....
.....
.....
.....

YAH:- MAELEKEZO YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA ELIMU YA MSINGI 2016/2017

1. **UTANGULIZI.**
   Uongozi na Jumuiya yote ya Chuo cha Ualimu Mandaka wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Stahahada ya Elimu ya Msingi katika Chuo hiki. Hongera sana! Ni tunu kupata nafasi ya kuchaguliwa kujiendeleza katika taaluma ya ualimu ambayo ni taaluma mama ya taaluma nyingine zote. Itumie vema nafasi hiyo ili katika kipindi chako cha mafunzo uweze kujijengea maarifa, stadi na mwelekeo wa kutosha kukidhi mahitaji ya mwalimu bora katika viwango vya sasa na baadaye katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa kwa ujumla.

   Mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Elimu ya Msingi yameandaliwa kwa lengo la kuwajengea umahiri wa kitaaluma na kitaalamu waalimu watakaofundisha katika Elimu ya Msingi, ili kumudu ufundishaji malezi ya wanafunzi, utafiti wa Kielimu na uendeshaji wa shule kwa ufanisi.

   Mafunzo haya ni ya miaka mitatu **(3)** na unatakiwa kuripoti Chuoni kuanzia tarehe **01 Novemba, 2016.** Na mwisho wa usajili ni tarehe **07** Novemba, **2016,** unatakiwa kufika Chuoni ndani ya tarehe hizo zilizotajwa bila kukosa.

1. MAHALI CHUO KILIPO NA USAFIRI WA KUKUFIKISHA CHUONI

a) Mahali chuo Kilipo

Chuo cha Ualimu Mandaka kipo mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Moshi Vijini.

b) Jinsi ya kufika Chuoni

- Ukiwa unatokea njia kuu ya Arusha/Moshi, elekea kituo kikuu cha mabasi, panda mabasi (hiace) yanayoenda Himo/holily/mwika/Marangu/kilema na uteremke kituo cha Himo mjini.
- Ukitokea njia kuu ya Tanga/DSM teremka stendi kuu ya mabasi ya njiapanda na panda gari zinazoelekea Himo mjini.
- Kutoka Himo mjini, panda magari yanayoelekea **Kilema** kwa **Lazari** na teremka kituo cha **Mandaka.**

Dira na Moto wa Chuo

- **Dira ya Chuo**: Kuandaa Waalimu bora watakaohimili ushindani wa soko la ajira kwa kutumia mbinu bora na za kisasa za ujifunzaji na ufundishaji.
- **Moto wa Chuo**: Taaluma usafi na uzalishaji mali.

2. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

a) Vyeti na hati za utambulisho.

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uje na vyeti halisi na halali vifuatavyo:-

i. Vyeti vya Taaluma (Academic Certificates) vya kidato cha IV au/na VI au hati ya matokeo (Result Slip) kwa ambao vyeti vyao havijatolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
ii. Vyeti vya Ualiumu Daraja la III.
iii. Vyeti vya kuhitimu (Leaving Certificates) vya Shule/Chuo cha Ualimu ulichosomea.
iv. Cheti cha Kuzaliwa (Birth Certificate).
v. Hati yoyote ya ziada inayoweza kusaidia kukutambulisha na kuthibitisha uhalali wako na uhalali wa umiliki wa nyaraka zako za Kitaaluma na Kitaalamu.
vi. Barua ya mwajiri inayothibitisha kuwa umepewa ruhusa ya kuja masomoni (Release Latter).

b) Ada.

Ada ya Mafunzo kwa mwaka ni Shilingi **600,000/=** unaweza kulipa yote au kulipa shilingi **300,000/=** kwa muhula. Fedha hii ya ada tu ilipwe kwenye Banki ya NMB Tawi la **Nelson Mandela Akaunti Na. 4031000023**. Jina la Akaunti **Mandaka Revenue Collection**.

c) Michango.

Kila mwombaji wa Mafunzo ya Ualimu aliyechaguliwa ili asajaliwe anatakiwa kulipa michango ifuatavyo:-

1. Mchango wa huduma ya kwanza ni Tsh. 10,000/=

2. Mchango wa UKarabati wa samani, majengo na miund mbinu ni Tsh. 10,000/=
3. Kitambulisho Tsh. 5,000/=
4. Mchango wa ulinzi Tsh.5,000/=
5. Gharama za usajili Tsh. 5,000/=
6. Fedha za kukodisha Godoro Tsh. 10,000/= kwa mwaka
7. Fedha ya mahafali Tsh.5,000/= kwa mwaka
8. Mchango wa michezo Tsh. 5,000/=
9. Mchango wa vazi la mahafali (Kukodisha Joho) Tsh.10,000/=
10. NACTE: Uthibiti Ubora (Quality Assurance Fee) Tsh. 15,000/=
11. Mchango wa Serekali ya wanachuo (MUWATA) Tsh. 5,000/=
12. Ada ya Mtihani: Kila mwanachuo atakayesajiliwa atatakiwa kulipa ada ya mtihani ya Tsh. 50,000/= kwa mwaka kwa ajili ya gharama za mitihani.

    Malipo ya michango mingine yote kuanzia namba 1-12 hap juu ilipwe kwenye benki ya NMB Tawi la **Nelson Mandela Akaunti Na. 4031000055**, Jina la akaunti **Pricipal Mandaka**

N.B. Kwa malipo yote ya ada na michango utakayolipa Benki, hakikisha una hati halisi ya kulipia fedha hizo (Bank Pay In Slip) tumia jina la mwanachuo kama lilivyoandikwa kwenye vyeti ambavyo utakuja navyo Chuoni ili upewe risiti ya malipo. Tafadhali zingatia tofauti ya akaunti ya ada na michango kama zilivyotajwa hapo juu. **Hatupokei fedha Taslimu.**

d) Sare ya Chuo

1. **Sare ya Chuo Wasichana:** Jozi/Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari (light blue), Suti nyeusi; Sketi na koti la mikono mirefu, tai ndefu ya blue yenye mistari myeupe. Kwa wasichana wa Kiislamu hijabu iwe kitambaa cha kichwa cheusi kisiwe na urembo wa aina yoyote, (Nunua kabla ya kuripoti Chuoni).
2. **Sare ya Chuo Wavulana:** Jozi/Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari (light blue), Suti nyeusi; Surali na koti la mikono mirefu, tai ndefu ya blue yenye mistari myeupe. Suruali iwe na luksi kwa ajili ya kufungia mkanda, marinda mawili kila upande, iwe na mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma wenye kifungo, chini iwe na pindo la kugeuzia (turn up).

   N.B: Sare ya chuo inaweza kushonwa katika maeneo ya karibu na chuo baada
   ya kufika chuoni.
3. **Sare ya viatu kwa wote.**

   Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu, visiwe na visigino virefu, Jozi mbili za soksi nyeupe kwa wasichana na bluu/nyeusi kwa wavulana.

   NB: Utatakiwa kuvaa Sare ya Chuo na mavazi NADHIFU na ya HESHIMA yatakayoendana na Maadili ya Ualimu wakati wote.

   Sare ya Chuo isiwe ya **Mtumba.**

4. **Mavazi ya michezo**

Truck suit, T-shirt yenye nembo ya Chuo na raba, ambapo Truck suit inapatikana chuoni kwa Tsh. **25,000/=** na T-shirt kwa Tsh. **12,000/=** mwanachuo atahitajika kuja na raba za michezo.

5. **Mahitaji kwa ajili ya mavazi.**

Shuka mbili rangi ya bluu bahari "light blue" kwa wanaume, shuka mbili rangi ya "pink" kwa wasichana, "bed cover" nyeupe, mto na foronya mbili nyeupe, chandarua nyeupe/bluu ya kuzuia mbu ft 3, blanketi moja zito, pazia zito rangi nyeupe kwa ajili ya dirisha la chumba utakachokuwa unalala.

6. **Mahitaji ya lazima kwa ajili ya Taaluma**

- Unahitajika kununua/kuja na Mihtasari ya maomo yanayofundishwa shule za msingi, pamoja na masomo ya shule za msingi visivyopungua vitatu.
- Counter book 13 Q2
- Mafaili kumi (File folder) ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za kitaaluma
- Bunda (ream – nopa) moja ya karatasi 500 za photocopy A4 zitapatikana duka la chuo.

7. **Afya**

a) Ili uweze kukubaliwa kusomea Mafunzo ya Ualimu unahitajika kupimwa afya yako na kuhibitishwa na Daktari wa Serikali kwa kujaza fomu (Request for Medical Examination) iliyoambatanishwa ambayo utakuja nayo Chuoni. Hakikisha kuwa fomu hiyo imepigwa muhuri wa Ofisi ya Daktari mhusika. Aidha, unaweza kuhitajika na mkuu wa Chuo kupimwa afya yako wakati wowote unapokuwa chuoni.

b) Mwanachuo mwenye uja uzito hatapokelewa chuoni.

c) Kwa kupitia mchango wa matibabu utakaotoa unapojiunga na baadae kila mwaka, chuo kitatoa huduma ya kwanza katika Zahanati ya chuo.

d) Chuo hakina uwezo wa kutoa huduma ya chakula maalu (Light or Special diet) kwa wanachuo wenye matatizo kiafya.

8. **Mahitaji Mengine**

Vifaa vya usafi:- Hard broom, soft broom, Squeezer, toilet brash, hard brash.
Mahitaji mengine madogomadogo kama vyombo vya chakula, matumizi ya photocopy na zana za kufundishia utajinunulia mwenyewe ufikapo chuoni baada ya kupewa maelekezo. Hakikisha una fedha za matumizi binafsi zisizopungua laki moja (Tshs 100,000).

N.B. Vifaa vya usafi binafsi vinapatikana kwenye duka la chuo.

9. **Kanuni na Taratibu**

Mwisho.

Kumbuka kuwa siku zote mwalimu anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa matendo mazuri na wanafunzi wake na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo kila mwanachuo anatazamiwa awe na tabia nzuri na mwenendo unaoakisi maadili ya Ki-ualimu wakati wote wa Mafunzo yake na baada ya Mafunzo yake, Jumuiya ya Chuo cha Ualimu Mandaka inakukaribisha Kujiunga na Mafunzo ya Ualimu.

UWE NA MAANDALIZI MEMA YA KUJA CHUONI

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MANDAKA.

Msemo.

Msemo, T. W. - Namba ya Simu:-**0754542635**

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MANDAKA
S. L. P. 725
MOSHI

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer.
.....
.....

FROM: Mandaka T.C,
P.O.Box 725
MOSHI.

Ref: Mrs. /Mr. Miss.....

Please examine the above named as to his/her physical mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I – III). Each category or sub-category of which will render the applicant in eligible in case of a effect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate in eligible for the course, including category V:-

I. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Speech
   (d) Lambs
   (e) Venereal diseases
   (f) Leprosy
   (g) Peptic ulcers
   (h) Epilepsy

II. Neuroses
III. Other serious diseases
IV. Pregnancy
V. Mental and Physical Fitness

PART B:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ and mentally fit for a full time teacher training course.

I. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (c) Speech
   (e) Venereal diseases
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
   (h) Peptic ulcers
II. Neuroses.....
III. Other serious diseases.....
IV. Pregnancy.....
V. Mental and Physical Fitness.....

Date .....Signature.....Station.....

Designation.....

Delete as necessary

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TECHNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MANDAKA

KANUNI ZA CHUO

UTANGULIZI

Mwalimu anatakiwa kuwa na tabia nzuri, mwadilifu, mbunifu na nadhifu wakati wote.

Ni wajibu wa Mwalimu kujitahidi kuielewa siasa ya nchi, kulipenda Taifa lake na kuwa tayari kulitumikia.

Zifuatazo ni Kanuni za Chuo cha Ualimu Mandaka ambazo ni lazima zifuatwe hapa Chuoni na wakati wa Mazoezi ya kufundisha (BTP) ili mwanachuo na walezi waweze kuyafikia malengo ya Chuo na Taifa kwa ujumla.

1. UTII NA HESHIMA

i. Kila mwanachuo anawajibika kutii sheria za nchi na kanuni za kazi ya Ualimu.
ii. Kila mwanachuo anawajibika kutii kanuni za chuo.
iii. Kila mwanachuo aheshimu alama kuu za Taifa ambazo ni Bendera, Wimbo wa Taifa na Nembo ya Taifa.
iv. Kila mwanachuo ajiheshimu mwenyewe na kuwaheshimu wanachuo wenzake, wafanyakazi na watu wengine.
v. Kila mwanachuo asishiriki katika matendo au kauli ambayo italeta aibu na kuvunja heshima yake au ya mwingine.
vi. Kila mwanachuo aheshimu na kufuata ratiba ya siku na ratiba ya masomo kwa kuhudhuria vipindi, mazoezi, majaribio na mitihani.
vii. Kelele haziruhusiwi katika mazingira ya chuo
viii. Ni marufuku kwa mwanachuo kutumia simu ya mkononi darasani, kwenye vikao na maeneo yote ambayo ni rasmi bila ruhusa.

2. KUTHAMINI SHUGHULI ZA CHUO

i. Kila mwanachuo awahi kufika katika sehemu ya kazi na kuondoka baada ya kukamilisha kazi kwa kuruhusiwa. Kila mwanachuo aheshimu na kushiriki katika kazi za uzalishaji mali kwa juhudi na maarifa.
ii. Kila mwanachuo aheshimu na kushiriki katika kazi za usafi atakazopangiwa.
iii. Kila mwanachuo aheshimu na kushiriki katika michezo na utamaduni kadri itakavyoonekana inafaa.

3. KUTUNZA MALI YA UMMA NA BINAFSI

i. Kila mwanachuo anawajibika kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinahifadhiwa salama katika sehemu zinazostahili
ii. Kila mwanachuo asipoteze, asichafue, asiharibu wala "**Asiibe**" mali ya Umma au ya mwanachuo mwenzake, au ya mtu yeyote.
iii. Kila mwanachuo anayepoteza au kuharibu kifaa au vifaa atalazimika kulipa thamani yake au kufidia.

iv. Kila mwanachuo anahusika na ulinzi wa Chuo kwa hiyo atoe taarifa kwa utawala wa chuo kuhusu vitendo au watu anaohisi wanahatarisha usalana chuoni.

4. HAIBA

i. Kila mwanachuo anatakiwa kuvaa sare ya chuo ikiwa safi na ya heshima anapokuwa darasani, anaporuhusiwa kutoka nje ya chuo, mikutanoni (Baraza) na kwa wakati wowote kadri atakavyoelekezwa. Mavazi yoyote yanayobana na kuonyesha maungo ya mwili na milegezo hayaruhusiwi kuvaliwa hapa chuoni.
ii. Kila mwanachuo ajiweke katika hali ya usafi wa mwili na mavazi wakati wote.
iii. Kila mwanachuo haruhusiwi kufuga kucha na kuzipaka rangi, kupaka rangi mdomo na macho, kuvaa mapambo kama herein, mikufu, shanga, bangili, kanga, vitambaa, pete, zisizoruhusiwa akiwa katika sare ya chuo.
iv. Kila mwanachuo anaruhusiwa kuwa na nywele fupi za kuchana au kusuka mitindo ya kuelekea kisogoni au kufunga kuelekea kisogoni, anapokuwa katika sare ya chuo.
v. Kila mwanachuo haruhusiwi kuvaa viatu vyenye kisigino kirefu, kandambili au makatambuga, nguo za kulalia au nguo za michezo wakati anapoingia darasani, katika ukumbi wa chakula au vikao rasmi, au anapoitwa na mlezi, au kutoka nje ya chuo.
vi. Ni marufuku kwa mwanachuo kutia madawa makali nywele zake mf. curl, relaxer n.k ndani ya Bweni kwani yanaathiri afya za wanachuo wenzake.

5. RUHUSA

i. Mwanachuo lazima apate kibali cha maandishi cha ruhusa kutoka kwa mkufunzi wa Zamu, mwadili au Mkuu wa Chuo kabla ya kutoka nje ya mipaka ya chuo.
ii. Ruhusa ya kwenda hospitali ya Kilema, Zahanati ya Umoja na sehemu za karibu na chuo itatolewa na Mkufunzi wa Zamu, ruhusa ya kwenda mjini na sehemu zilizo mbali na chuo itatolewa na Mwadili. Ruhusa ya kulala nje ya chuo itatolewa na mkuu wa Chuo kwa mwanachuo kuandika barua baada ya kuonana na mwadili wa wanachuo.
iii. Mwanachuo anayeruhusiwa kutoka nje ya chuo ataandikwa kwenye daftari la ruhusa na anatakiwa arudi saa 10:00 jioni na kuweka sahihi kitabuni kwa Mkufunzi wa zamu au ofisi inayohusika.
iv. Mwanachuuo haruhusiwi kutembelea nyumba za wakufunzi au wafanyakazi wasio waufunzi bila ruhusa ya Mkufunzi wa Zamu, Mwadili au Mkuu wa chuo.
v. Kila mwanachuo anapaswa kuwa na kitambulisho popote anapokuwa
vi. Ruhusa ya kwenda nyumbani – msiba n.k itatolewa kwa mzazi/mlezi, mtoto, ndugu wa kuzaliwa na kwa mume/mke. Ruhusa ya kutoka nje ya chuo itatolewa mara mbili kwa mwezi (siku za wikiendi).

6. UHUSIANO NA MAWASILIANO

i. Kila mwanachuo azingatie kwamba uhusiano kati ya mwachuo ni kama uliopo kati ya kaka na dada.

ii. Kila mwanachuo awe na uhusiano wa wafanyakazi kama ule wa mtoto na wazazi au walezi wake.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kuwa katika uhusiano wa kimapenzi na Mkufunzi au Mfanyakazi yeyote asiye Mkufunzi au Mwanafunzi mwenzake.
iv. Mwanachuo atambue ngazi za mawasiliano kati yake na mwanachuo mwenzake au viongozi, na kati yake na walezi na Mkuu wa Chuo
v. Si ruhusa wanachuo wa kike kutembelea mabweni ya wavulana na wavulana kutembelea mabweni ya wasichana.
vi. Kila mwanachuo atatakiwa kuwa ndani ya Bweni lake saa mbili na nusu usiku ikiwa hakuna umeme.

7. AFYA

i. Kila mwanachuo anawajibika kuyaweka mazingira yake nje na ndani katika hali ya usafi kama bwenini, bwalo la chakula na viwanja n.k.
ii. Wanachuo wagonjwa wafike Zahanati kuanzia saa 12:30 – 1:30 alfajiri kutibiwa
iii. Wanachuo wanaoruhusiwa kwenda Zahanati ya Umoja na Hospitali ya Kilema, waandike katika madaftari yatakayojazwa na daktari na wapate kibali cha kutoka kwa Mkufunzi wa zamu, baada ya kuorodhesha majina yao, wale wanaoruhusiwa kwenda Hospital ya Mawenzi na KCMC wapate kibali cha ruhusa kutoka kwa Mwadili
iv. Wanachuo waripoti kwa Mkufunzi wa Zamu wanaporudi na pia waeleze matibabu yao ya rufaa kwa Matron ambaye atamwarifu Mwadilifu, Mkufunzi wa zamu au Mkuu wa chuo juu ya waliopata E.D au maelezo maalumu kwaajili ya ufuatiliaji wa matibabu ya mwanachuo anayehusika.
v. Mwanachuo asitume taarifa yoyote ya ugonjwa kwa Mzazi au Mlezi bila Uongozi wa chuo kujua. Taarifa yoyote kama ni lazima itatolewa na Mkuu wa Chuo.
vi. Mwanachuo haruhusiwi kunywa pombe wala kuvuta sigara au madawa yeyote ya kulevya.

8. CHAKULA

i. Kila mwanachuo atagawiwa na kula chakula katika bwalo la chakula akiwa amekaa mezani kwa muda uliopangwa.
ii. Mwanachuo haruhusiwi kupeleka chakula bwenini.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kujipikia chakula bwenini.
iv. Chuo hakitoi chakula maalumu (Special diet).
v. Mwanachuo haruhusiwi kununua vyakula vinavyopikwa nje ya utaratibu wa chuo na anatakiwa kuepuka uchafu katika sehemu zote zinazohusika na chakula.

9. WAGENI

i. Mwanachuo haruhusiwi kutembelewa na wageni siku za masomo.
ii. Mwanachuo haruhusiwi kumpeleka mgeni yeyote bwenini, darasani, dukani, maktaba, jikoni n.k bali amkaribishe katika ukumbi wa mikutano.

iii. Mwanachuo lazima atoe taarifa kwa mkufunzi wa zamu na mwenyekiti wa zamu mara apatapo mgeni.
iv. Mwanachuo anaweza kutembelewa na wageni kila jumapili kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 10:00 jioni.

10. ADHABU

Mwanachuo akivunja mojawapo ya kanuni za mwenendo bora anaweza kupewa adhabu na kiongozi wake, Mkufunzi, Mkuu wa chuo, Kamati ya Nidhamu au Baraza la Wakufunzi, Bodi ya Ushauri ya chuo kutegemea na uzito wa kosa na adhabu inayostahili kutolewa ambayo yaweza kuwa:-

i. Kufanya kazi za nje kwa muda mrefu zaidi au kwa muda wa ziada
ii. Kuzuiwa kutoka nje ya chuo kwa kipindi Fulani
iii. Adhabu yoyote ambayo kiongozi ataona inafaa kumrekebisha mkosaji au kuwafundisha wengine.
iv. Kusimamishwa masomo kwa muda.
v. Kufukuzwa chuoni kabisa.